# TUSHIRIKISHANE

## TONE la URENDO



**TOLEO LA MWEZI OKTOBA - 2023**

# DIBAJI

Toleo hili la Tushirikishane linakuja baada ya muda mrefu ndio maana tunashirikishana matukio ambayo tayari yameshapitwa na Wakati. Lakini tusisahau kuwa, licha ya kuwa na lengo la kuhabarishana, matoleo haya yanatuwezesha kuweka kumbukumbu ya matukio muhimu katika maisha ya Province yetu. Lengo letu ni kuja kuyaweka katika chapisho moja la kila mwaka ili yabaki katika historia ya Shirika letu. Kadiri muda unavyopita ndivyo maisha yetu na jinsi tulivyoishi Karama na Tasaufi yetu hujenga desturi ambazo wenzetu watakaokuja baadaye wataweza kujua urithi tunaowaachia.

Hivyo basi katika Toleo hili tunawakumbusha matukio yafuatayo:

- Upadrisho w mwaka huu 2023 wa Wamisionari wenzetu Bernard Kasambala Hezron, Alphons Martin Fataki na Faustine Barnabas Missanga uliofanyika mwezi Januari.
- Kupokelewa rasmi na kwa daima kwa Wamisionari wapya kumi na mmoja na kupewa daraja Takatifu la Ushemasi
- Maadhimisho ya Jubilei ya fedha ya mapadre wetu wane na Junbilei ya dhahabu ya Pd. William Mnyagatwa.
- Tukio la kifo cha Mpendwa wetu Pd. Richard Orota nalo ni tukio ambalo haliwezi kusahaulika.
- Mwisho tunawajulisha mabadiliko kadhaa katika mpangilio ya maishi ya Jumuiya katika Province yetu.



# WAMISIONARI WATATU WAPADRISHWA MWEZI JANUARI



Mwezi wa Januari mwaka huu 2023 ulikuwa mwezi wa baraka kwa Province yetu ya Tanzania kwa sababu Alphons Fataki cpps, Bernard Kasambala cpps na Faustine Missanga cpps, walioingia kwa daima Shirikani na kupewa daraja la Ushemasi mwezi Julai 2022, Walipadrishwa, kila mmoja katika jimbo lake la asili.

Aliyekuwa wa kwanza kupadrishwa alikuwa S**hemasi Bernard Kasambala** mnamo tarehe 12 Januari kwenye Parokia ya Mwenyeheri Anwarite - Butonga Rungwe – Jimbo Katoliki la Mbeya. Ibada iliyoongozwa na Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga iliadhimishwa kwa shangwe kubwa kwa sababu Padre Bernard ndiye padre wa kwanza katika Parokia ya nyumbani kwake.



Katika mahubiri yake akichukua kutoka Isaya 61: 1-3, alifafanua wajibu wa Kuhani. Askofu Mkuu Nyaisonga alisisitiza jinsi kazi hizo zinavyotimizwa na kwa kutoa maoni yake juu ya injili ya Mathayo (Mt. 9, 35-38). Alisema tuna kielelezo kizuri cha Yesu ambaye alizunguka katika miji na vijiji vyote, akifundisha katika mazingira yao na kuhubiri habari njema ya Ufalme, akiponya kila ugonjwa na udhaifu. Kwa hili alimsihi padre mpya asichague mahali pa kwenda kwa ajili ya huduma bali awe tayari kutumwa kila mahali. Pili, alisema

kwamba Yesu alichochewa na huruma na kujali mahitaji ya watu. Aliona watu walioteswa na wanyonge kama kondoo wasio na mchungaji, ndivyo inavyopaswa kuwa roho ya kila Padre. Kuhani ni mtu ambaye shughuli zake za uchungaji hazisukumwi na fedha, wala vitu, bali kwa kuangalia mahitaji ya watu wa Mungu. Alihitimisha mahubiri yake kwa kuwaasa waamini kuwaunga mkono mapadre katika huduma yao, lakini pia waonyeshe ufahamu wa kasoro zao, kwa sababu wao si malaika, bali ni wanadamu wenye karama na makasoro, kwani tunajua, kama asemavyo Mtume Paulo "tuna hazina ya Mungu katika vyombo vya udongo" (2Kor. 4,7).

Siku iliyofuata, Jumamosi Januari 13, Fr. Bernard Kasambala aliadhimisha Ibada ya Misa Takatifu katika Kanisa la Parokia hiyo ikifuatiwa na tafrija na mashangilio yaliyohudhuriwa na watu wengi waliofika kumpongeza kwa zawadi ya hiyo upadri.

Wa pili kupadrishwa alikuwa ni **Shemasi Alphons Fataki** katika Kanisa kuu la Kwiro Mahenge siku ya Ijumaa tarehe 19 Januari na aliyempa daraja hilo takatifu ni Askofu Agapitus Ndorobo Askofu wa Jimbo Katoliki Mahenge. Kabla ya kuwekwa wakfu Ask. Ndorobo alitoa mahubiri mafupi ya kumsihi Shemasi Fataki juu ya yafuatayo: Awali ya yote alisema kuwa Ukuhani ni zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajili ya Kanisa, hivyo kuna haja ya kuwa na shukrani na unyenyekevu katika kuwatumikia watu wa Mungu. Pili alimsihi awe kuhani karibu na moyo wa Mungu kwa sababu kama vile tawi lililounganishwa na mti halinyauki viyo hivyo tawi lililokatwa katika mti hakika litakauka (Yn 15, 1-2). Hivyo basi kuhani anayekaa ndani ya Mungu daima atabaki kuwa kuhani mwema. Tatu, alimuhimiza Padre mpya kuwa kama chumvi na



mwanga kati ya watu wa Mungu kwa njia ya maisha yake ya sala,

kwa ukarimu na uchapakazi.

Ibada hiyo ya Upadrisho ilihudhuriwa na Mapadre wengi, Watawa wa kiume na kike kutoka sehemu mbalimbali za Jimbo la Mahenge, Ifakara, Morogoro na maeneo mengine ya nchi. Siku iliyofuata, Jumamosi Januari 20, Fr. Alphons Fataki aliadhimisha Misa ya shukrani nyumbani kwa shangwe nyingi, maburudisho tele na ngoma za asili licha ya mvua kubwa iliyonyesha mchana huo.

Wa tatu kupadrishwa alikuwa **Shemasi Faustine Missanga,** adhimisho hilo lilifanyika siku ya Ijumaa tarehe 27 Januari, katika Parokia ya Damu ya Azizi Itigi. Ingawa Parokia ya nyumbani kwa Faustine ni Makiungu, iliamuliwa kuwa na maadhimisho haya katika Parokia yetu ya Damu Azizina Askofu Edward Mapunda ndiye aliyeongoza ibada hiyo. Askofu Mapunda alikuwa ameandaa mahubiri mafupi yaliyosisitiza mambo yafuatayo juu ya huduma ya kipadre. Kwamba kuwa Kuhani ni zawadi kutoka kwa Mungu (Ebr. 5, 1-10), ni ishara ya upendo na huruma ya Mungu, kwa hiyo kuhani ni mhudumu wa huruma na upendo wa Mungu. Pili, Kuhani ni mtumishi, hivyo anadaiwa unyenyekevu na uaminifu (Yn. 15, 9-17). Ukuhani si kazi bali ni huduma ya maisha yote ambayo haina uhusiano wowote na utukufu wa kidunia. Tatu, alimsihi padre mpya kukabidhi maisha yake kwa Moyo mtakatifu wa Yesu ambaye kutoka kwake tunajifunza upole na uaminifu. Nne, alimkumbusha Padre mpya asijisahau kwamba yeye ni kiumbe dhaifu na mwenye dhambi, hivyo maisha yake ya kila siku yanapaswa kutafuta utakatifu pamoja na watu wa Mungu. Mwisho, aliwasihi waamini walioshiriki liturujia hiyo waendelee kumuombea Padre mpya ili awe mtumishi mwema na mwaminifu.



Siku iliyofuata - Jumamosi Januari 28, tulisafiri hadi Makiungu, kwenye Parokia iliyoko kilomita 70 kutoka Itigi ambako jumuiya ya Parokia ya eneo hilo ilikuwa imemwandalia karamu kubwa. Misa hii ya shukrani ilihudhuriwa na mapadre wa jimbo la Singida, Wamisionari kutoka jumuiya mbalimbali nchini Tanzania, Walei washirika wanaojulikana kwa jina la Utume wa Damu kutoka Dar-es-salaam, Morogoro Dodoma na jumuiya ya wenyeji.

Mapadre wetu wapya wamepangiwa vituo vya utume kama ifuatavyo: **Fr. Bernard Hezron** ameendelea kufanya utume wake katika **Parokia ya Bk. Maria Mkingiwa dhambi ya Asili Kinda Morogoro**, pia ameendelea kuwa mlezi mwandamizi wa vijana wetu kwenye mwaka wao wa pili wa malezi. **Fr. Alphonce Fataki** yeye amepangiwa kufanya kazi kwenye **Parokia yetu ya Mt. Yohana Paulo II Shanwe Mpanda. Fr. Faustine Missanga** amepangiwa utume kwenye **Parokia ya Mt. Nikolaus Mtongani (Kunduchi)**, na pia ameteuliwa kusimamia shule yetu ya Ufundi hapo hapo Mtongani.



# INCORPORATION NA USHEMASI WA VIJANA KUMI NA MOJA



Mwaka huu Shirika letu limewapokea rasmi na kwa daima vijana kumi na mmoja katika Shirika na kufanya idadi yetu kuwa 102. Frt. Abelhad Ismail Dimosso Mzaliwa wa Tegetero Morogoro; Frt. Aidan Alphonce Mtui Mzaliwa wa Mbahe Aris Moshi; Frt. Abibon Lawrent Rukiza Mzaliwa wa Kemondo Bukoba; Frt. Appolonius Ludovick Byarugaba Mzaliwa wa Nshamba Kagera; Fr. Bonaventure Aquiline Maro Mzaliwa wa Kishimundu Moshi; Frt. Ernest August Shirima Mzaliwa wa Tarakea Rombo Kilimanjaro; Frt. Gregory Ndeshillo Mzaliwa wa Mrao Rombo Kilimanjaro; Frt. James Titus Makinda Mzaliwa wa K/Ndege Dodoma; Frt. Joseph Richard Msumeno Mzaliwa wa Kambikatoto Chunya Mbeya; Frt. Livinus Ndamwesiga Benedicto Mzaliwa wa Maruku Bukoba; Frt. Revocatus Charles Gimbuya Mzaliwa wa Simiyu.

Misa ya kuwapokea rasmi na kwa daima ilifanyika katika Kanisa la Seminari yetu (St. Gaspar College) Morogoro jioni ya tarehe 7 July 2023. Misa hiyo iliongozwa na Mkuu wa Shirika Province ya Tanzania Fr. Vedasto Ngowi na kuhudhuriwa na idadi kubwa ya Mapadre na Watawa wanaoishi na kufanyakazi maeneo ya Morogoro.

Akiongozwa na masomo ya ibada ya misa kwa heshima ya Damu Azizi Fr. Vedasto aliwatafakarisha yafuatayo kuhusu ukuu na upekee wa hatua ambayo vijana hawa wameichukua. Kwanza kabisa alisema kuwa tendo lao la kuweka wakfu maisha yao kwa Bwana rasmi na kwa daima ni tendo kubwa na la ujasiri. Toka leo vijana hawa wanakaza uso wao kwa Bwana wakihamasishwa na Damu ya thamani sana ambayo aliitolea msalabani, alisema jambo hili sio mzaha.



Akiongozwa na masomo ya siku Fr. Vedasto alisema tunaalikwa kutafakari juu ya Damu hiyo ambayo ni Damu ya Msalaba na damu ya Kikombe. Katika kutafakari ujumbe wa masomo ya Misa Fr. Vedasto anasema tunaalikwa kutafakari utimilifu wa Agano la Kale – yaani damu ya wanyama iliyotolewa altareni na kunyunyiziwa watu kwa utakaso – imekuja kukamilika katika Damu aliyoitoa kwa upendo mkubwa Yesu pale msalabani. Kama vile Yesu alivyosulibiwa nje ya mji wa Yerusalemu ndivyo anavyotuelekeza kwamba damu yake imemwagika kwa ajili ya hali na watu waliotengwa na kudharauliwa katika mazingira mbalimbali. Huko ndiko Vijana wanaopokelewa katika Shirika linaloitwa la Damu azizi ya Yesu, wanakotumwa kwenda kupeleka faraja na wokovu. Aliwasiisitizia kuchukua utume watakaoupewa kuwa ni wa kupeleka damu ya Msalaba na pia damu ya kikombe, sio kama kuwadanganya watu kwa faraja za miujiza bali kuwasimika kwa imani kwa Bwana ambaye ndiye tegemeo la maisha yao.

Mwishoni aliwasisitizia kuwa katika tendo la kupokelewa Shirikani wanafanya agano na Mungu kwamba watakinywea kikombe cha damu ya Msalaba ambacho pia ni kikombe cha mateso, kikombe cha Baraka, kikombe ambacho kitawaletea ushindi katika maisha yao ikiwa watakuwa waaminifu kwa agano wanaloliweka. Katika ibada hiyo walipewa ishara ya kwamba wao ni wanashirika, alama hiyo ni Msalaba wa kimisionari. Maneno ambayo yalitamkwa wakati wa kupewa msalaba huo yana maana kubwa katika maisha yao: “Pokea msalaba huu ambao ndio alama ya kuwa wewe ni Mwanashirika. Uyaige yatokanayo na msalaba huu, uwatangazie watu wa Mungu Neno la Wokovu, ili waweze kubaki waaminifu katia Agano Jipya na la milele lililoratibishwa kwa Damu ya Kristo. Msalaba huu utakaouvaa uwe alama ya Kristo aliye hai na anayeishi ndani ya moyo wako. Hivyo uupende msalaba huu na uukumbatie, ujitoe kwa Kristo bila kujibakiza daima na popote, kwa njia ya msalaba huu, utukufu wa Baba wa mbinguni udhihirike ndani yako”.



**USHEMASI:** Siku iliyofuata, Jumamosi ya tarehe 8 July Wamisionari hao wapya kumi na mmoja walipewa Daraja Takatifu la Ushemasi. Ibada na madhehebu yaliongozwa na Askofu Lazarus Vitalis Msimbe askofu wa Jimbo Katoliki la Morogoro. Ibada ilifanyika katika maeneo ya kituo kipya cha vijana kilichojengwa kwa ajili ya utume wa vijana ili kukuza na kuhamasisha vipaji chini ya uongozi wa Fr. Reginald Lyamuya. Watu wengi walifurika, wakiwemo Mapadre na Watawa majirani toka maeneo ya Kola; lakini kwa namna ya pekee Wamisionari wa Damu Azizi walihudhuria kwa wingi kwa maana wengi walikuwa wanajiandaa kuhudhuria Mkutano mkuu wa uchaguzi ambao ulifanyika Dodoma kati ya tarehe 10 hadi 13 July.



Wakati wa Ibada ya Misa Takatifu Askofu Msimbe alisisitiza yafuatayo akitafakari toka Masomo ya Misa (Hes 3:5-9; Mdo 6:1-7; Lk 10:1-9): Kwanza kabisa aliwaasa Mashemasi watarajiwa kuzingatia kwamba Ushemasi sio cheo bali ni Huduma ndani ya Kanisa la Mungu. Hivyo basi aliwasisitizia wazingatie na kuwa mahiri katika huduma ya ibada na utume wa kuhudumia taifa la Mungu. Zaidi ya hayo aliwakumbusha yaliyosomwa kutoka somo la kwanza kuwa wajibu wao wa pili ni kutunza Matakatifu, kuandaa vyema ibada ili huduma yao hiyo iweze kuwaongoza watu kumkaribia Mungu. Tatu aliwakumbusha kuwa kama vile Mashemasi wa kwanza walivyoteuliwa kati ya watu wema na wenye busara, inawapasa hata hawa wateule watimize huduma ya ushemasi na utume wao kwa busara na hekima. Mwisho aliwahimiza kudumu katika wito wao kwani kama somo la Injili lilivyotukumbusha kwamba "mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache" (Lk 10:2). Ask. Msibe alibainisha kuwa Kanisa, shirika na jamii ya waamini inahitaji wahudumu wa Injili, ukitilia maanani kuwa miito katika Kanisa



ulimwenguni imepungua, hivyo wakidumu waaminifu katika wito wao watatekeleza yale ambayo Kristo mwenyewe aliwaagiza wafuasi wake.

Baada ya adhimisho la misa Takatifu yalifuata mashangilio na mlo wa pamoja na wageni wengi walitoka sehemu mbalimbali za Tanzania, ukitilia maanani kwamba walikuwepo wageni wa kila shemasi. Mkuu wa Shirika aliwatangazia kwamba kila Shemasi ataendelea kufanya utume kwenye kituo ambacho alikuwa anafanyia mazoezi ya kichungaji.














# TUMKUMBUKE

## FR. RICHARD LEONE OROTA:

Siku ya Jumatatu tarehe 7 Agosti mwaka huu ilikuwa siku ya huzuni sana tulipopata habari za kifo cha Padre Richard Orota. Simanzi kwa wengi wetu zilitokana na kwamba Pd. Orota baada kuugua kwa muda mrefu karibu miaka miwili alishapata nafuu na afya yake ilikuwa ikiboreka siku hadi siku. Wote tulikuwa na matumaini kwamba atapona kabisa na kuendelea na utume wake kama mwanzo.




Wengi wetu tulionana naye wakati wa sherehe zake za Jubilei ya fedha zilizofanyika katika Parokia ya Mwenyeheri Isdori Bakanja Boko tarehe … na baadaye tulimwona wakati wa Mkutano mkuu wa Uchaguzi pale Dodoma. Lakini hasa wengi wa watu wake wa karibu walikuwa wamemwona baada ya Mkutano Mkuu alipopita karibu kila nyumba ya Shirika kuwashukuru kwa sala za uponyaji na kuwaalika kwenye sherehe yake ya nyumbani.

Lakini tusemeje, ila kukubali mapenzi ya Mungu, maana kama asemavyo Nabii Isaya: *"Mawazo yangu si kama mawazo yenu, wala njia zangu si kama njia zenu. Kama vile mbingu zilivyo mbali na dunia, ndivyo njia zangu zilivyo mbali na zenu, na mawazo yangu mbali na mawazo yenu"* (Isa 55:8-9). Mungu aliyekuwa amemponya na kumrudisha wima ndiye aliyehitaji asherehekee Jubilei yake ya fedha katika utumishi kama Padre huko Mbinguni.



Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha na wito wa Fr. Richard Leone Orota. Mungu alimjalia karama nyingi njema alizozishiriki na watu wengi amabao waliishi na kufanya utume naye. Fr. Orota. Alikuwa mcheshi na mchangamfu hata wakati alipokuwa anapitia hali ngumu ya afya. Alifanya kazi zake za kitume kwa weledi na bidii, alikuwa na karama ya pekee ya ucheshi. Pia usafi na unadhifu kama Mt. Gaspari, tena likuwa na jicho la pekee kwa kutunza mazingira, kupanda miti kutunza nyumba alikopitia na ndivyo alivyowajali watu aliowahudumia. Apumzike kwa Amani.











# JUBILEI YA MIAKA 25 NA 50 YA UPADRE WA WAMISIONARI 2023



Ilikuwa Shangwe, vifijo na nderemo, mnamo tarehe 17 mwezi August Katika Parokia ya Mt. Nicholaus Kunduchi Mtongani ambapo Wamisionari wa Damu Azizi ya Kristo walipokuwa wanamshukuru Mungu kwa miaka 25 ya Upadre wa **Pd. Leonidas Ntampera, Pd. Seventine Banulirwa, Pd. Richard Orota na Pd. Alfons Minja.** Lakini pia katika adhimisho hilo tuliungana na **Pd. William Mnyagatwa** ambaye alikuwa akimshukuru Mungu kwa miaka 50 ya Upadre. Katika adhimisho hilo nia ya pekee ilikuwa kumwombea pumziko la milele **Pd. Richard Orota** ambaye alifariki dunia siku kumi kabla – yaani tarehe 7 Agosti. Katika adhimisho hilo alikuwepo Pd. Benedetto Labate, cpps ambaye naye alipadrishwa pamoja na wale wanaoadhimisha mika 25 ya Upadre! Pd. Benedetto ni Mhasibu wa Shirika Province ya Italia, na aliambatana na baba yake mzazi Mzee Antonio Labate.

Adhimisho hilo la Misa Takatifu liliongozwa na Askofu Mkuu Yuda Thadeus Ruwa'ichi, OFM Cap., Askofu wa Jimbo kuu la Dar es salaam. Mapadre wengi Wamisionari wa Damu Azizi walishiriki lakini pia Vicar General wa Jimbo kuu na baadhi ya Mapare wa Jimbo na Mashirika mabalimbali. Waumini wengi wa Parokia ya Kunduchi Mtongani na Parokia za jirani walihudhuria kuwashangilia na kuwapongeza Wana Jubilei, hasa kundi la WanaUtume wa Damu Azizi ya Kristo.

Katika mahubiri yake, Askofu Mkuu Yuda Thadeus katika kutafakari neno la Mungu alisisitiza yafuatayo: Kwamba kama vile Musa alivyoteuliwa na Mungu kuwaongoza Waisraeli toka utumwani Misri, vivyo hivyo

Wanajubilei wameteuliwa kuwa Makasisi wa Mungu, bila mastahili yao. Aliwahimiza Waumini kuwaombea ili waendelee kutimiza majukumu yao kwa uaminifu kama walivyo fanya hadi sasa, ili Mungu awaimarishe, waendelee kuwatakatifuza watu, kuwafundisha na kuwaongoza wafike kwa Mungu. Kwamba kama vile Injili ilivyoelekeza (Mt. 18:21 – 19:1) Makasisi ni wajumbe wa Msamaha, huruma na upatanisho na Mungu. Hivyo basi kwanza kabisa wao wenyewe wajipatanishe na Mungu siku kwa siku; pili kwa kuwa wao ni vyombo vya huruma ya Mungu, wanaitwa kupeleka huruma ya Mungu kwa watu na kuwapatanisha wao kwa wao na wao na Mungu.



Picha ya pamoja Askofu mkuu Yuda Thadei Ruwa'ichi, Mkuu wa shirika la Damu Azizi Pd. Vedasto Ngowi pamoja wa wajubilanti wa Miaka 25 na 50 ya Umisionari.

# APPOINTMENTS AND TRANSFERS

## PD. ALESSANDRO MANZI:



Tarehe 18 mwezi Agosti mwaka huu Pd. Aless andro Manzi aliondoka nchini kwenda Cesena Italia. Toka mwaka jana Pd. Alessandro aliandika barua kwa Provincial akiomba kwenda kushughulikia matibabu ya afya yake akiwa karibu na daktari wa familia. Baada ya kusikia habari hizo, Askofu wa Cesena aliomba Shirika ili Fr. Alessandro afanye utume atakapokuwa pale. Askofu amemkabidhi utume katika Parokia ya Sta Maria Nuova. Anwani yake ni Via S. Croce 4076 – 47023 Bertinoro – Cesena Italia. Pd. Alessandro atatambulishwa rasmi katika Parokia hiyo mpya siku ya Jumapili tarehe 5 Novemba. Pamoja na utume huo Pd. Alessandro atakuwa Legal Administrator wa parokia jirani na pia ni Decano wa eneo hilo ambalo lina Parokia saba. Utume huo anaufanya akiwa bado ni mwenzetu katika Province, hivyo basi tumwombee aweze kukamilisha matibabu yake na kufanya utume vema katikaJimbo la Cesena. Email yake ni aleman70@libero.it na namba yake ya simu ni +39 333 178 1539.

## PD. REGINALD MROSO:



Mwezi wa Agosti Provincial alimteua Pd. Reginald Mrosso na kumpendekeza kuwa Paroko wa Parokia ya Mkiwa. Pd. Mrosso amekuwa mratibu wa mradi wa uchimbaji wa visima vya maji (Water Project kwa zaidi ya miaka nane. Baada ya kuteuliwa rasmi na Askofu wa Singida Pd. Reginald alihamia Mkiwa tangu mwanzoni mwa mwezi Agosti na kutambulishwa rasmi kwa wanaparokia tarehe 6 August katika Sikukuu ya kun'gara sura Bwana.

## PD. EUGENE NCHIMBI:



Kama wote tunavyojua Fr. Eugene alirudi toka Italia mwezi July mwaka jana (2022) kwa shida ya afya ya wazazi wake. Alipangiwa majukumu katika miradi ya Shirika – St. Gaspar Hotel & Conference Center, Radio Mwangaza, Shule zetu za Gaspar na John Merlini na Mradi wa uchimbaji visima vya maji. Mwaka huu, kwa barua ya tarehe 5 January Atlantic Province kwa kupitia Msimamizi ya miradi (Director of Development and Mission Projects) aliteuliwa kuwa Deputy Mission Director. Majukumu yake ni kusimamia utendaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Atlantic Province nchini Tanzania. Fr. Eugene ni kiunganishi kati ya Province ya Tanzania na Atlantic.

## PD. DR. OSCAR MAKALA:



Mwezi August mwaka huu Fr. Dr. Oscar Makala aliondoka kwenda Kampala Uganda ambako ameanza masomo ya Uzamili katika taaluma ya Upasuaji. Dr. Makala alimaliza Shahada yake ya kwanza mwaka 2016 na kuanza rasmi kazi mwaka 2017 katika Hospitali ya Mt. Gaspari Itigi. Alipata nafasi ya kwenda nchini Italy kufanya masomo ya uzoefu wa Upasuaji na hasa fani ya urekebishaji wa ngozi (Plastic and Maxillofacial surgery) katika Hospitali ya Watoto ya Bambin Gesu – Roma Italy. Alimaliza masomo hayo na kurudi Tanzania mwaka 2021. Dr.Oscar Makala ameanza rasmi masomo yake tarehe 24 Agosti 2023, kule Kampala International University akichukua Shahada – Master of Medicine in Surgery. Kozi yake itachukua miaka mitatu.

## PD. BENJAMIN MWINUKA:



Kama mnakumbuka, Fr. Benjamin baada ya upadrisho mwaka 2021 alipangiwa kufanya utume katika Parokia ya Boko katika Jimbo kuu la Dar es salaam. Mwaka huo mwezi wa Agost alitumwa nchi Italia kuchukua masomo ya Tauhidi ya kiroho na Malezi katika Chuo Kikuu cha Kipapa cha Mt. Gregory Mkuu mjini Roma. Mwezi

Juni mwaka huu amehitimu masomo hayo na kwa sasa ameteuliwa kuwa Baba wa Kiroho na Mlezi mwandamizi katika nyumba yetu ya Malezi ya Mtumishi wa Mungu Yohani Merlini – Miyuji. Tunamtakia utume mwema na uliotukuka katika majukumu yake haya mapya.



# MATANGAZO:

**Wasimamizi wa Districts:** Kufuatia Uchaguzi wa Uongozi wa Province yetu, imeonekana kuna umuhimu wa kila District kuwa na Mhamasishji kutoka toka safu ya Uongozi wa Province kama ifuatavyo. Dar es salaam – Fr. Dominic Mwaluko; Morogoro – Fr. Achileus Mutalemwa; Dodoma – Fr. Richard Kungi; Manyoni – Fr. Felix Mushobozi.

- Katika kikao cha Halmashauri ya Shirika kilichofanyika tarehe 26 July, iliamuliwa kuunganisha pia jumuiya ambazo ziko mbali na Kanda zetu nne asilia. Iliamuliwa kuwa Jumuiya ya Gunyoda iambatanishwe na Kanda ya Dodoma; Benaco na Old Maswa wanaweza kuunda Kanda ya Ziwa na Fr. Paul Ngayomela akaungana na Kanda hii. Jumuiya ya Mpanda itaunganishwa na Kanda ya Manyoni. Angalau mara kwa mara inabidi wafanye jitihada za kukutana na wenzao hasa wakati wa Pasaka, Krismasi, au Sherehe muhimu za Shirika, lakini pia kunapokuwa na suala la kujadiliwa.

  Pia iliamuliwa kuwa Wamisionari wanaotoa huduma katika maeneo ambayo hakuna jumuiya za CPPS wajiunge na jumuiya zilizo karibu nao. Hivyo basi Fr. Paul Ngayomela atakuwa wa Old Maswa;
  Fr. Denis Mlimira atakuwa wa CPPS Makao Makuu Kisasa,
  Fr. Richard Tiganya atakuwa wa Jumuiya ya Boko na Fr. Chesco Msaga atakuwa mwanajumuiya ya Procura.

- Frt. Wilbrant Urio kupokelewa Shirikani tarehe 12 January 2024 na kupewa daraja la Ushemasi tarehe 13 January 2014.

- Mashemasi wetu kumi na mmoja watapewa Daraja Takatifu la Upadre tarehe 13 January 2024 Kwenye Parokia ya Bk. Maria Malkia wa Damu Azizi Kisasa Jimbo Kuu la Dodoma.

**“Maoni na mapendekezo juu ya toleo hili yanakaribishwa ili kuboresha habari zetu”**

Wasiliana na Pd. Felix Mushobozi, C.PP.S

P.O BOX 932 DODOMA

cppstzprovince@gmail.com

+255 653 475 366
+255 769 415 585

www.preciousbloodtz.or